

# SHIRIKA LA MAENDELEO YA PETROLI TANZANIA (TPDC)



## TAARIFA KWA UMMA

Kufuatia taarifa kwa umma ya tarehe **2 Januari 2018** iliyotolewa na Kampuni ya Swala Oil and Gas (T) Plc juu ya nia ya Kampuni yake Tanzu (Swala (PAEM) Ltd kununua hisa za Kampuni ya PanAfrica Energy Corporation (PAEM), Shirika la Maendeleo ya Petroli Tanzania (TPDC) kama mmiliki wa leseni zote za utafiti na uzalishaji wa mafuta na gesi hapa nchini mnamo tarehe **19 Januari 2018** ilitoa taarifa kwa umma ikiufahamisha kutokuwa na taarifa za kutosha kuhusiana na mchakato wa uuzaji wa hisa hizo.

Taarifa kwa Umma iliyotolewa na TPDC ilitokana na ukweli kwamba Kampuni ya PAEM ambaye ndiye muuzaji wa hisa anatajwa kuwa mmiliki wa kampuni ya PanAfrica Energy (T) Ltd (PAET) kampuni ambayo ni mkandarasi wa kitalu cha Songo Songo na anatajwa kumilikiwa kwa asilimia 100%.

Ifahamike ya kwamba mnamo mwaka 2001, Serikali, TPDC na PAET waliingia Mkataba wa Ugawanaji Mapato (PSA) katika kitalu cha Songo Songo kwa ajili ya uzalishaji na uendelezaji wa gesi ya ziada (Additional gas). Aidha ikumbukwe kwamba TPDC ndiye mmiliki wa vitalu vyote vya utafiti na uzalishaji wa mafuta na gesi

hapa nchini kwa mujibu wa Sheria ya Petroli ya Mwaka 2015.

Taarifa ya TPDC ya tarehe **19 Januari 2018** ililenga kuueleza Umma juu ya uamuzi wa Serikali kusitisha biashara hiyo kufanyika hadi hapo Serikali itakapojiridhisha juu ya mchakato huo. Hii inatokana na mawasiliano ya awali yaliyofanyika baina ya TPDC na ORCA Exploration Group Plc kwa barua ya tarehe **19 Disemba 2017** ORCA Exploration Group Plc ilikana kuwepo kwa uuzaji wa hisa baina ya PAET na mnunuzi yeyote. Vile vile barua hiyo ilieleza kwamba PAET hauzi sehemu ya umiliki katika mradi wa Songo Songo.

Hata hivyo kwa mujibu wa taarifa mbalimbali zinazotolewa na viongozi wa kampuni ya Swala, zimekuwa zikibainisha kuwa ununuzi huo wa hisa utaifanya kampuni ya Swala kuwa na ushiriki ndani ya Kitalu cha Songo Songo. Kwa vile TPDC ni mmiliki wa leseni ya Kitalu cha Songosongo, anawajibika kuwa na taarifa zote zinazo husiana na jambo lolote linaloweza kuwa na athari kwenye utekelezaji wa masharti ya leseni ya kitalu hicho.

TPDC ipo tayari kwa mazungumzo na muwekezaji yeyote atakayependa kuja kuwekeza katika sekta ndogo ya mafuta na gesi hapa nchini kwa kufuata sheria na taratibu za nchi.

*TPDC kwa Maendelo ya Taifa*

*Imetolewa na;*

Kaimu Mkurugenzi Mtendaji

Shirika la Maendeleo ya Petroli Tanzania Benjamin

William Mpaka Pension Towers

S.L.P 2774

**Dar es Salaam.**

Tovuti: [www.tpdc.co.tz](http://www.tpdc.co.tz)